

SHIRKI NA AINA ZAKE

SHIRKI ni mja kumfanyia Mwenyezi mungu kuwa kuna mungu mwininge kinyume ya Allah katika ulezi wake, uungu wake na katika majina yake na sifa zake.

SHIRKI ZIKO AINA MBILI : Shirki kubwa - Shirki ndogo

SHIRKI KUBWA.

Shirki kubwa ni kufanya aina yeyote ya ibada kinyume na Allah (sw), na mwenye kufanya shirki atakaa motoni milele ikiwa atakufa bila ya kutubia kwa Allah.

Shirki inabatilisha matendo mema ya mtu, Allah anasema :

قال تعالى: ﴿وَلَوْ أَشْرَكُوا بَحْتَهُ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾ [الأسماء: ٨٨]

("Na lau kama watamshirkisha mwenyezi mungu, basi yatapomoka yote waliyokuwa wakiyafanya") (Al-Anam: 88).

Na shirki kubwa mwenyezi mungu haisamehe isipokuwa mtu mpaka atubie toba ya kisawasa.

قال تعالى: ﴿إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرِكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ وَمَنْ يُشْرِكُ بِاللَّهِ فَقَدِ افْتَرَى إِثْمًا عَظِيمًا﴾ [النساء: ٤٨]

Allah anasema: ("Hakika ya Allah hasamehe dhambi ya kushirkishwa, na anayasamehe madhambi mengine yasiyokuwa shirki, na mwenye kumshirkishwa mwenyezi mungu kwa hakika amezua dhambi kubwa sana") (An-nisah: 48).

Miongoni mwa aina za kubwa ni kuomba kwa asiyekuwa mwenyezi mungu, au kuweka nadhiri kwa asiyekuwa mwenyezi mungu, au kuchinja kwa asiyekuwa mwenyezi mungu, na vinginevyo, au kufanya kwa asiyekuwa mwenyezi mungu miungu mingine na kuipenda zaidi ya Allah (sw).

قال تعالى: ﴿وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَتَّخِذُ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَنْدَادًا يُجْبِيُهُمْ كَحْبُ اللَّهِ﴾ [البقرة: ١٦٥]

(Wako miongoni mwa watu wanachukua badala ya mwenyezi mungu miungu mingine, wakiwapa mapenzi kama wanavyo mpenda mwenyezi mungu) (A-Baqarah:165).

AINA YA PILI YA SHIRKI NI SHIRKI NDOGO.

Shirki ndogo ni ile ambayo imeelezwa kwenye quran au hadithi za Mtume Muhammad (saw) akaisema kuwa ni shirki lakini ikawa haijafika kiwango cha shirki kubwa.

Shirki hii ndogo haimtoi mtu katika uislamu tofauti na shirki kubwa, lakini inapunguza kupwekesha Allah, kama vile mtu kuwa na Riya, na kauli ya kusema ametaka mwenyezi mungu na wewe, na kusema lau sikama mwenyezi mungu na wewe, pia kuapa kwa asiyekuwa mungu, bila ya kuitakidi kuwa kinachoapiwa kinanufaisha au kinadhuru kinyume ya mwenyezi mungu.

Pia kusema kuwa akitaka mwenyezi mungu na kutaka Fulani basi jambo hili lingekuwa hivi hivi n.k.

لقول النبي ﷺ: ((أَخْوَفُ مَا أَخَافُ عَلَيْكُمُ الشَّرُكُ الْأَصْغَرُ)) ، فُسْئِلَ عَنْهُ، قَالَ: ((الرِّيَاءُ)) [رواه أحمد وإسناده جيد]

Mtume (saw) anasema : (Kitu cha kuwahofisha zaidi juu yenu ni Shirki ndogo, aksarizwa Mtume ni ipi hiyo? Mtume akasema ni Mtu kuwa na Riya) (Ameipokea Imamu Ahmad na Mapokezi yake ni mazuri).

وقوله ﷺ: ((مَنْ حَلَفَ بِغَيْرِ اللَّهِ فَقَدْ أَشْرَكَ)) [رواه أبو داود: ٢٨٢٩]

Mtume (saw) anasema : (Mwenye kuapa kinyume ya mwenyezi mungu, kwa hakika amefanya shirki) (Amaipokea Imam Abu Daud : 2829).

Matendo yanayofungamana na shirki ndogo ni kufunga Hirizi, kufunga bangili au uzi kwa lengo la kukuondolea madhara au kukukinga na maradhi pamoa na matatizo, lakini mtu akaitakidi kuwa inanufaisha au kudhuru na kwamba sio sababu ya kudhurika au kunufaika, basi hiyo itaingia kwenye shirki kubwa.